turathi zisizogusika

United Nations
Educational, Scientific and
Cultural Organization

KITENGO CHA TURATHI ZISIZOGUSIKA
www.unesco.org/culture/ich

TOLEO LA MESSENGER LA TURATHI ZISIZOGUSIKA

SEPTEMBA 2006

ISSN 2071-7784



**TOLEO MAALUM: *Lugha Zilizo Hatarini***

Utangulizi:Masuala ya Lugha ........ uk. 1 na 8
Lugha Zilizo Hatarini na UNESCO ........ uk. 2
Mtazamo wa Mkataba ........ uk. 3
Nyanjani ........ uk. 4
Kinachoangaziwa: Afrika ........ uk. 6
Ujumuishi ........ uk. 7
Uchapishaji ........ uk. 8

✦ Zaidi ya asilimia 50 ya lugha 6700 za ulimwengu ziko katika hali ya hatari kubwa na zina uwezo wa kupotea kuanzia kizazi cha kwanza hadi cha nne.

✦ Asilimia 96 ya lugha ulimwenguni zinazungumzwa na asilimia 4 ya jumla ya idadi ya watu ulimwenguni.

✦ Nusu ya lugha zote hupatikana katika nchi nane pekee: Papua New Guinea, Indonesia, Nigeria, India, Mexico, Cameroon, Australia na Brazil.

*Ulimwengu ni mpangilio wa kimtazamo uliopambika na kila mtazamo umezingirwa na lugha. Kila mara lugha inapopotea, mtazamo mmoja wa dunia unapotea.*
David Crystal, Mwanalugha wa kutajika

Tarakimu zozote zilizotolewa katika *Messenger* ni makadirio na yako wazi kwa mjadala.

# Masuala ya Lugha

***Rieks Smeets****, Kitengo cha Turathi Zisizogusika*

Toleo hili maalum la *Messenger* limejikita katika Mpango wa UNESCO wa Lugha Zilizo katika Hatari ya Kuangamia, mojawapo ya shughuli muhimu za Kitengo cha Turathi Zisizogusika. Zaidi ya kuendeleza malengo ya Maafikiano ya 2003, mpango huu unajumuisha sehemu muhimu ya mpango mpya wa UNESCO ulioundwa na sekta mbali mbali kuhusu masuala ya lugha.

Kama tunavyoijua lugha, huenda ilistawi miaka isiyozidi 150,000 iliyopita katika Afrika Mashariki na kisha kupenyeza katika sayari. Wataalam wanakubali kwamba milenia au vikwi kadha vilizopita idadi ya lugha kote ulimwenguni ilikuwa juu zaidi kushinda makadirio ya lugha 6,700 zinazokisiwa kuwa leo. Katika karne zilizopita, idadi ya lugha imekuwa ikipungua kwa sababu ya upanuzi wa kiuchumi na kitamaduni katika nchi chache zinazotawala, ubora wa lugha zao na kwa ujenzi wa nchi - taifa. Katika miongo ya hivi karibuni, kupungua huko kumeongezeka sana kwa sababu ya mambo ya kisasa na utandawazi.

Kwa nini lugha ni muhimu? Kama njia kuu na ya kimsingi katika mawasiliano ya binadamu, lugha huwa hazitoi ujumbe pekee; pia hueleza hisia, nia na thamani, kuthibitisha uhusiano wa kijamii na kuonyesha masuala ya tamaduni, kijamii na desturi. Katika hali yake ya kuzungumzwa, kuandikwa, ama kwa ishara, lugha ndicho chombo cha kumbukumbu, tamaduni, maarifa na ujuzi. Pia, lugha hujumuisha na husaidia katika kutambua watu binafsi na makundi ya watu. Uhifadhi wa lugha za jamii za ulimwengu huchangia kupanua uanuwai wa utamaduni, ambao UNESCO inachukua kama maadili muhimu ya kuendeleza ustawi katika ulimwengu wa sasa ambao unaendelea kuwa katika utandawazi.

Je, lugha zote zinafaa kuhifadhiwa? Kama vyombo vinavyoishi, lugha zinabadilika kila wakati: zinakua, kugawanyika, kuungana na wakati mwingine kufa. Kuangamia kwa lugha huenda kukaonekana kama jambo la kawaida. Lugha zimekuwa zikichanganyika na kusaidiana kama inavyodhihirishwa na lugha mbili ama zaidi katika maeneo mengi kote ulimwenguni. Kimsingi, lugha zote ikiwa ni pamoja na lugha za ishara, ni sawa: baadhi yake zina misamiati mikubwa, nyingine huenda zikajivunia tamaduni za muda mrefu, lakini kila lugha imetayarishwa vilivyo kushughulikia mawasiliano na mahitaji yanayohusiana ya wazungumzaji wake na pia kukumbatia maendeleo mapya. Inayamkinika kwamba hakuna lugha moja ambayo ni bora inayoweza kufanywa kuwa lugha inayotawala. Mipango ya kuandika lugha inaweza kuundwa, misamiati kupanuliwa na kichakata-matini kuundwa kwa kila lugha. Hatimaye, uokoaji wa lugha hutegemea pakubwa uamuzi na msukumo wa kisiasa, sera, mipango na ufadhili.

Ama kwa kweli, sio lugha zote zinaweza kulindwa.
*(inaendelea kwa ukurasa wa mwisho)*



© Discovery Communications, Inc.

*Bunuba, lugha ya wenyeji wa Ki-australia wa Ki-Aborigin, haina zaidi ya wazungumzaji 100 waliobakia, wengi wao ni wakongwe. Wazee wa Bunuba hujaribu kuelimisha watu kuhusu lugha ya mababu zao kwa kutoa hadithi kama ilivyofanywa katika siku za nyuma.*

***Kulia**, Kadazandusun huzungumzwa na takribani watu 300,000 wa Sabah, huko Malaysia. Baada ya kutishwa na lugha hiyo kupungua kwa kasi, jamii ilichukua hatua na kuanzisha Kituo cha Lugha na mafunzo ya mara kwa mara ya lugha.*




© Discovery Communications, Inc.



© Discovery Communications, Inc.

***Juu**, wazungumzaji wa lugha ya Toba wako takribani 15,000 huko Argentina. Tamaduni za 'Watoba' zina utajiri wa mila na maarifa ya masuala ya uasili hasa yanayopokezwa kutoka kizazi hadi kizazi kupitia kwa hadithi na nyimbo.*




## Kuchunguza Uthabiti wa Lugha za Kiasili

Ripoti ya Kitaifa ya Uchunguzi wa Lugha za Kiasili 2005, iliyotayarishwa na Taasisi ya Australia ya *Aboriginal na Torres Strait Islander Studies* kwa ombi la Serikali ya Australia, inatoa ukaguzi wa hali ya lugha za kiasili za Australia kulingana na msingi wa UNESCO kuhusu uthabiti wa vigezo tisa vya lugha (tazama grafu). Miongoni mwa mambo muhimu iliyopata, ripoti hiyo ilibainisha kwamba ni lugha 145 pekee kati ya 250 za kiasili zinazojulikana Australia ambazo zinaendelea kuzungumzwa. Zaidi ya hayo, takriban lugha 110 kati ya hizo zimeorodheshwa kama zilizo kwenye hatari ya kuangamia. Ni lugha 18 za kiasili ambazo zimetajwa kama "zilizo imara" kuambatana na kipengee hicho muhimu kinachotumika kama kibadilishi kati ya kizazi kimoja kwa kingine.

Kwa habari zote za ripoti ya Uchunguzi ya Australia, tufikie kupitia: www.dcita.gov.au/indig/maintenance_indigenous_languages/publications

# Lugha Zilizo kwenye Hatari ya Kuangamia na UNESCO

## Mpango unaolenga kulinda turathi za lugha na upanuzi wake

Ijapokuwa wapo wataalamu wachache wa lugha waliokuwa na maono mazuri na kuwazia kuufahamisha umma kwa jumla kuhusu hatari ya kuangamia kwa lugha tokea hata miaka ya 1970, ni hivi majuzi tu ambapo mataifa ya ng'ambo yamelichukulia umuhimu suala hilo. Katika kipindi cha mwanzo wa miaka ya 90', mafunzo maalum na makongamano yaliitishwa ili kuanza kulishughulikia suala hilo, na maamuzi ya kuwepo kwa miradi ya kubadilisha mawimbi hayo ilipoanzishwa. Katika miaka ya mapema ya 1993 ndipo idara ya shirika la UNESCO kupitia kwenye Kitengo cha Turathi Zisizogusika ilipozindua mradi wa kitabu chake kilichofahamika kama – Mradi wa Kitabu cha Lugha Zilizo katika Hatari ya Kuangamia, yaani *The Red Book of Languages in Danger of Disappearing* na kile cha - Afisi ya Kimataifa ya Lugha Zilizo katika Hatari ya Kuangamia kutoka Chuo Kikuu cha Tokyo mnamo 1995. Mwaka uliofuatia, UNESCO ilichapisha toleo la kwanza la, Kitabu cha Lugha za Ulimwengu Zilizo katika Hatari ya Kuangamia - '*Atlas of the World's Languages in Danger of Disappearing*" (tazama Ukurasa wa 8 kwa habari kamili).


Kwa habari zaidi tufikie katika: http://www.tooyoo.l.u-tokyo.ac.jp/Redbook

Katika Kitengo cha UNESCO cha Turathi Zisizogusika, Mpango wa Lugha Zilizo Hatarini unalenga kuchangia katika uimarishaji wa kulindwa kwa upanuzi wa lugha tofauti tofauti kote ulimwenguni kupitia kwa:

- Kuhamasisha umma kuhusu lugha kuwa hatarini kupitia machapisho na vyombo vya habari;
- Kuboresha na kuimarisha juhudi za kawaida za kuendeleza mbinu za kuandika na kuhifadhi lugha ambazo hazijaandikwa;
- Kuhakikisha ushiriki wa jamii zinazoongea lugha fulani katika shughuli za kulinda ama kufufua lugha zao;
- Kutambua na kusambaza matumizi bora katika uhifadhi wa lugha;
- Kutetea ushirikiano wa kimataifa kupitia mikutano ya wataalamu na mitandao ya mawasiliano.

### Mbinu ya Kukagua Hatari ya Kuangamia kwa Lugha

Ili kuweza kuamua kuhusu hatua maalum za ulinzi, mtu lazima afafanue; ni nini maana ya hatari ya kuangamia kwa lugha fulani? Na ni kwa kiwango gani lugha hiyo iko katika hali ya hatari?. Mnamo 2002 na 2003, UNESCO iliuliza kundi la wanalugha wa kimataifa kuunda mpango wa kupima uthabiti wa lugha. Kikundi hiki cha dharura cha wataalam kilichohitajika kushughulikia hali ya hatari ya kuangamia kwa lugha, kilitoa ripoti ya uchanganuzi wa maono muafaka iliyofahamika kama, Ustahamilivu wa Lugha na Hali ya Hatari ya Kuangamia kwake - "Language Vitality na Endangerment", na ambayo iliunda vigezo tisa vifuatavyo:




Hakuna sababu hata moja itakayotosheleza ukaguzi wa lugha ya kijamii. Hata hivyo, zikichukuliwa pamoja sababu hizi tisa zinaweza kuamua uthabiti wa lugha, kazi yake katika jamii na aina ya hatua zinazohitajika kwa usimamizi ama uboreshwaji wake.

Kwa habari kamili ya ripoti hiyo, tufikie kupitia: www.unesco.org/culture/en/endangeredlanguages/languagevitality



© Renato S. Rastrollo/NCCA

# Mtazamo wa Maafikiano

## Maafikiano ya 2003 yanatambua lugha kama chombo cha Turathi za Tamaduni Zisizogusika (ICH)

Maafikiano ya Kulinda Turathi za Tamaduni Zisizogusika , ambayo yalianza kutekelezwa Aprili 20, 2006, yaliundwa ili kulinda turathi zilizopo za binadamu huku yakiimarisha ubunifu wa binadamu, upanuzi wa tamaduni, pamoja na maslahi ya makundi na jamii ambazo zinaendesha mafundisho na masuala yanayojumuisha turathi hizi.

Ingawaje waandishi wa Maafikiano haya bila shaka walichukua lugha kama jambo muhimu katika turathi za tamaduni zisizogusika 'ICH' bila wasiwasi wowote, sehemu ya sheria haitoi nafasi ya ulinzi wa lugha kikamilifu. Kweli, kulingana na ufafanuzi uliotolewa katika Kifungu cha 2, orodha isiyo na vikwazo ya ICH inajumuisha "mila za masimulizi na pia hisia, ambazo ni pamoja na lugha kama chombo cha turathi za tamaduni zisizogusika". Na kwa hali hiyo, Maafikiano yanatambua jukumu muhimu la lugha katika hisia na usambazaji wa 'ICH'. Na zaidi ya hayo, vitengo vyote vya 'ICH' - kuanzia mila na masuala ya kilimwengu hadi kwa matambiko na bidhaa za uchongaji - vinategemea lugha kwa desturi yao ya siku baada ya siku na usambazaji kati ya vizazi. Kadhalika, hali za kuitambua jamii na makundi zinaangaziwa katika misamiati ya lugha zao. Mojawapo ya vitengo vilivyoelezwa katika Maafikiano - vile vya mila za masimulizi na hisia - vinategemea lugha sio kwa usambazaji na utekelezaji pekee bali pia kwa maelezo yake binafsi.

Suala la lugha kama chombo cha turathi za tamaduni zisizogusika na hasa mila za masimulizi na hisia, lilijadiliwa kwa kina katika mkutano wa wataalamu ulioandaliwa Januari 2006 kwa madhumuni ya kuelezea siku za usoni *Mwongozo wa Kulinda Mila za Masimulizi na Hisia*. Mwongozo huu umepangwa kuchapishwa mnamo mwaka wa 2007, na utakuwa wa kwanza katika mpangilio wa vitengo maalum vya mwongozo ambao umeundwa kusaidia Mataifa Wanachama wa Maafikiano hayo pamoja na mataifa mengine, wanachama wa jamii na mashirika yasiyo ya serikali katika kuendeleza na kutekeleza hatua za ulinzi na shughuli za utimizaji wa malengo ya Maafikiano hayo.



© Kyrgyz National Commission for UNESCO



© Renato S. Rastrollo/NCCA

***Picha mbili juu, 'Hudhud chants', Kito kilichotangazwa mnamo 2001, bado zinasomwa na watoto wa jamii ya Ifugao katika shule maalum za Hudhud.***

# Nyimbo za Hudhud za Jamii ya Ifugao

Hudhud ni mila ya masimulizi iliyo na zaidi ya miaka 700 wakati ambapo ilikaririwa na kuimbwa na jamii ya Ifugao ya Luzon Kaskazini wakati wa msimu wa kupanda, kuvuna mpunga na kesha za matanga. Masimulizi yanayodumu kwa siku kadha kwa kawaida huendeshwa na mwanamke mkongwe ambaye huwa kama mwanahistoria wa jamii na mhubiri. Kwa wakati huu, Hudhud iko kwenye hatari ya kuangamia; wasimulizi wachache waliobakia wanaelewa hazina yote na habari za kuandikwa ni chache kwa sababu ya ugumu wa kuandika lugha hii ya Ki-Hudhud.


Katika mwaka wa 2001, masimulizi ya nyimbo za Hudhud yalitangazwa kuwa Kito cha Masimulizi na Turathi Zisizogusika za Binadamu. Mradi uliozinduliwa na UNESCO mnamo 2003 kwa ufadhili wa Serikali ya Ujapani unalenga kuhakikisha kuenea, kuzungumzwa na kuimbwa kwa nyimbo za Hudhud kwa vizazi vipya vya watendaji. Mbali na kufunzwa katika shule maalum za Hudhud katika jamii ya Ifugao, utamaduni huo sasa umejumuishwa katika mtaala wa shule. Kadhalika, mashindano ya kukariri hufanywa ili kuinua Hudhud miongoni mwa umma kwa jumla. Shughuli za mradi pia zinajumuisha kukusanya, kuhifadhi nyaraka na kurekodi Hudhud.

***Usanii wa Akyns, utendi wa 'Kyrgyz epic tellers'- kito cha thamani kilichopatikana mnamo 2003 - kinaendelea kusambazwa kwa watu wadogo- Utendi wa kipindi cha katikati kwenye jamii ya Kyrgyz una utajiri wa zaidi ya miaka 1000, kwa sayansi ya watu wa Manas, huku wakiwazia mateso ya Manas pamoja na jamii na wafuasi wake.***

# Nyanjani

## Vidokezo vya miradi na shughuli zinazoendeshwa na Kitengo cha Turathi Zisizogusika kwa kuangazia lugha zilizo katika hatari ya kuangamia

© IEA, CASS



Kuna wazee karibu 20 pekee wanao ongea Hezhen waliobakia katika mkoa wa Heilongjiang, Uchina. Kwa sababu ya mawasiliano ya muda mrefu na watu wa lugha iliyokithiri ya Mandarin, lugha ya Hezhen inayoongewa leo ni mchanganyiko wa Hezhen na Mandarin.

### Kutoka kwa lugha za kuzungumzwa hadi kuandikwa

Wazungumzaji wa Bembele na Gbete, kabila mbili ndogo za jamii ya Niger-Congo zinazozungumzwa katika eneo la Bertoua Kusini-Magharibi mwa Cameroon wanaweza kutumia lugha zao katika sehemu zinazokubalika pekee kwani lugha hizo hazikuwa na mbinu ya kuandikwa. Tunatoa shukran kwa mradi wa kuhifadhi nyaraka ulioendeshwa na Kituo cha Utathmini wa Lugha cha NACALCO kilichoko mjini Yaounde. Vijana wawili kutoka Cameroon ambao ni wataalamu na wajuzi wa lugha, kwa ushirikiano wa karibu na wazungumzaji, walianzisha misingi ya kuandika na kutoa nyaraka za kutumiwa (mwongozo wa tahajia, miongozo ya ufundishaji, orodha ya maneno n.k) kwa lugha hizo mbili za kutumiwa katika madarasa ya lugha, uwililugha na elimu ya watu wazima na katika uandishi magazetini. Wajuzi hao pia waliwafunza wanachama hao wa kijamii kuwa kama wasaidizi wa lugha na walimu wa siku zijazo katika madarasa ya lugha. Tunapongeza kuwepo kwa vifaa vipya na mafunzo, wazungumzaji sasa wanaweza kupanga mradi na kuandaa mafundisho ya lugha katika jamii yao.

© NACALCO




*Katika kijiji Kusini- Magharibi mwa Cameroon, mwanamke anayezungumza Bembele anajifunza kusoma na kuandika lugha yake mwenyewe. Hii imewezeshwa kupitia jitihada za uhifadhi muhimu wa lugha na kuundwa kwa vifaa vya lugha.*

### Kuunga Mkono Wachina Katika Juhudi Za Kulinda Lugha Ndogo

Kirasmi, Uchina ina zaidi ya makundi 56 ya kikabila na wingi wa zaidi ya lugha 120 zilizopo leo, kuanzia kabila la Mandarin lenye karibu wazungumzaji bilioni 1 na lahaja karibu 100, mpaka kabila la Hezhen lenye karibu wazungumzaji 20 pekee. Kuanzia 2002 hadi 2005, Afisi ya UNESCO ya Beijing imeunga mkono Taasisi ya Ethnolojia na Anthropolojia (IEA) ya Chuo cha Uchina cha Sayansi za Kijamii (CASS) kuendesha rekodi na utafiti wa lugha nane ndogo zilizo katika hatari ya kuangamia huko Uchina: ***Manchu, She, Lakkia, Tujia, Yugur Magharibi, Anong, Hezhen na Ersu.*** Katika kila lugha, wataalam waliunda nyaraka muhimu sana (kamusi, sarufi, n.k) na vifaa vya mafunzo kusaidia ukuzaji wa lugha katika elimu. Mradi huo pia ulichangia kuundwa kwa hifadhi ya picha na maneno kwa matumizi ya wanaosomea elimu ya binadamu na wajuzi wa lugha.

Anwani: Ofisi ya UNESCO ya Beijing, Beatrice Kaldun, b.kaldun@unesco.org



© UPNG

*Kushoto, katika warsha ya jamii iliyoandaliwa na wanalugha kutoka Chuo Kikuu cha Papua New Guinea (UPNG), huko Honiara, Visiwa vya Solomon, wazungumzaji wa lugha ndogo wanajifunza jinsi ya kuhifadhi lugha zao ili waweze kuzitayarisha kwa matumizi makubwa.*



© APT

## Kulinda Upanukaji wa Uanuwai wa lugha huko 'Pacific'

Zaidi ya lugha 2000 zinapatikana katika eneo kubwa la 'Pacific', na nyingi hazijaandikwa. Kati ya mwaka wa 2000 na 2003, awamu ya kwanza ya mradi wa kufufua lugha uliendeshwa huko Papua New Guinea, Visiwa vya Solomon, Vanuatu na Fiji kuhusu kuhifadhi lugha ambazo hazijaandikwa kama Zia, Sare, Tape, Naman na Nese. Shughuli za utafiti ziliangazia kuunda uhifadhi wa kimsingi na vifaa vya lugha kusaidia katika utumiwaji mkubwa wa lugha hizi za kijamii, hasa katika elimu rasmi na ile isiyo rasmi. Mradi huo ulipokea msaada mkubwa kutoka kwa jamii-lugha ambazo zilihusika katika kazi ya uakibishaji wa lugha. Tunashukuru mno kwa matokeo ya kutia moyo ya mradi huu, Serikali ya Ujapani iliamua kufadhili awamu ya pili katika mwaka wa 2006/2007 kwa kuangazia lugha 12 za Papua Guinea, Visiwa vya Solomon na Vanuatu. Mradi huo utaendelea kusaidia kuhamasisha jamii: wanafunzi wanaoongea lugha hiyo na wafanyakazi wa nje ambao watafunzwa uakibishaji wa lugha ili kuhakikisha kwamba shughuli za mradi zinaendelezwa vyema.

## Ushirikiano kati ya UNESCO, *Discovery Communications, Inc.* na Mpango wa Kazi ya Umoja wa Mataifa

Kwa sababu ya kuelewa uwezo wa televisheni katika usambazaji wa habari kwa mamilioni ya watu ulimwenguni, Kitengo cha Turathi Zisizogusika kilifanya ushirikiano na kampuni ya *American Global Media, Discovery Communications, Inc,* katika utengezaji wa filamu zinazoonyesha jamii zinazoongea lugha zilizo katika hatari ya kuangamia. Mnamo mwaka wa 2003 na 2004, filamu fupi kumi na nane zilitengezwa na kuonyeshwa kimataifa katika kituo cha *'Discovery'* kilichoko katika nchi 160. Filamu hizo zinawajulisha watazamaji kuhusu changamoto zinazowakabili watu wanaozungumza lugha iliyo katika hatari ya kuangamia, kwenye maeneo ya: Argentina, Canada, Hindi, Ujapani, Malaysia, Mexico, Uingereza, Sweden, Autralia, Croatia, Gabon, Guetamala, Lithuania, Panama na Afrika Kusini.

Kwa habari zaidi wasiliana nasi kupitia:
www.unesco.org/culture/en/endangeredlanguages/discovery

## Kufufua tifinagh, maandishi ya kitambo sana ya Tuareg

Baadhi ya thuluthi-mbili ya takriban Watuareg 1.5 milioni wanaoishi Niger hutumia lugha yao ya kitamaduni, Tamajaq, kila siku. Ingawaje lugha yao ya kiasili ya WaTamajaq inayofahamika kama, Tifinagh, bado inaendelea kusambazwa, lakini huwa haitumiki sana huko Niger siku hizi. Kuanzia 2003 hadi 2006, UNESCO ilisaidia Chama cha Uimarishaji wa Tifinagh (APT) katika Agadez, Niger katika uchapishaji wa jarida la mara mbili kwa mwezi *Amanar*, vifaa kadhaa vya mafunzo na vijitabu kadhaa vilivyozingatia uhalisi wa tamaduni za uzungumzaji na hisia. Vifaa vyote vya kusoma vilichapishwa katika lugha za Tamajaq, Tifinagh na Kifaransa. Nakala 500 za kila kijitabu zilisambazwa kwa maktaba za vijiji na shule, na jarida liliuzwa kwa jamii za Tuareg, huko Niger kaskazini. Kadhalika, madarasa yaliandaliwa mnamo mwaka wa 2003 na kufunza Watuareg 2000 maandishi ya kale ambayo bado yanaonekana kama njia muhimu ya kuhifadhi kutambuliwa kwa lugha ya WaTuareg.

Kuzinduliwa kwa jarida na kusambazwa kwa vifaa vya kusoma kulivutia sana makundi ya WaTuareg katika Niger ambao sasa wanaweza kutumia Tifinagh kwa kiasi kikubwa.


## Rejesta ya UNESCO ya Mafunzo Bora katika Uhifadhi wa Lugha


Juhudi hizi za UNESCO zilizinduliwa mnamo mwaka wa 2006 na zinalenga kukusanya habari za ufanisi katika masuala ya kulinda lugha na kutoa mbinu za uvumbuzi, habari za kutegemewa na miundo kwa jamii zinazoongea kote ulimwenguni.

Maakaba haya, ambayo yanatarajiwa kuwa katika mtandao wa mawasiliano kufikia mapema mwaka wa 2007, yatajumuisha miradi ya kijamii katika nchi tofauti na kuangazia maeneo makubwa kama elimu, ufufuzi, uwekaji viwango, ustawi wa jamii, uhamasishaji, uhifadhi na utumiaji wa teknokolojia mpya.

Kwa habari zaidi au kuwasilisha mradi wasiliana nasi kupitia:
www.unesco.org/culture/en/endangeredlanguages/goodpractices

*Juu na Chini,*
*Jarida la Amanar linasambazwa kwa kutumia mgongo wa ngamia kutoka kwa kijiji kimoja hadi kijiji kingine na kutoka kwa shamba moja hadi kwa shamba jingine ili kufikia jamii za Tuareg, Niger Kaskazini. Jarida hilo limeandikwa kwa lugha ya KiTifinagh, maandishi ya kikale ya KiTuareg na pia Kifaransa.*







**FEBRUARY 21 SIKU YA KIMATAIFA YA LUGHA YA MAMA**

*Mtu haishi Kwa nchi, Bali huishi Kwa lugha.*
*Hiyo ndiyo nchi yetu, ardhi ya mama yetu - hakuna nyingine.* E.M. Cioran

FEBRUARY 21
International Mother Language Day

# Kwenye Mtazamo: Afrika




## Jitihada za UNESCO za Kuokoa Lugha Zilizo katika Hatari ya Kuangamia

Katika kipindi cha miongo mitatu iliyopita, nchi nyingi za Afrika zimefanya juhudi za kulinda lugha zao za kitaifa. Mifano ya kutia moyo inapatikana Afrika Kusini ambapo lugha 11 rasmi zinatumika kwa masuala ya kiusimamizi, katika mfumo wa elimu, vyombo vya habari n.k. Uhabeshi kwa sasa inatekeleza sera kabambe kwa kutumia lugha 22 za Uhabeshi katika elimu, kuanzia kiwango cha elimu ya msingi. Hata ingawaje kuna juhudi hizo, lugha nyingi za Afrika zimetishwa sana na juhudi za pamoja zinahitajika ili kuunda sera maalum za lugha na juhudi za ulinzi ambazo zinahimiza lugha nyingi na uhifadhi wa lugha nyingi za Afrika iwezekanavyo. Pingamizi kuu zinajumuisha ukosefu wa ufadhili na nia ya kisiasa pamoja na ukosefu wa uhifadhi wa lugha za Kiafrika.

Kwa sababu UNESCO inalipa bara la Afrika kipaumbele, Shirika hili limezindua miradi kadhaa inayozingatia lugha za bara hili. Mnamo 1997, kongamano la muungano kati ya serikali za Mataifa Wanachama kuhusu Sera za Lugha za Kiafrika, lililofanyika Harare, lilianzisha mipango na utekelezaji wa sera . *Hatua thabiti hazikufuatwa wakati wote.

Tunaonekana kuwa katika mwelekeo mpya sasa. Uamuzi kuhusu lugha za Afrika uliofanywa majuzi na Muungano wa Afrika (AU) unaonyesha kuongezeka kwa habari miongoni mwa waamuzi wa Afrika kuhusu jukumu muhimu linalochangiwa na lugha za Afrika katika maendeleo. Mkutano Mkuu wa marais wa AU huko Khartoum ulitangaza 2006 kuwa "Mwaka wa Lugha za Kiafrika" na kuteua taasisi ya *African Academy of Languages (ACALAN)* kuwa mratibu wa sera za lugha na mipango katika bara la Afrika na mshauri maalum kwa Mataifa Wanachama katika uwanja huu.

* Ripoti kamili ya mkutano itatolewa na Kitengo cha Turathi Zisizogusika kufikia Septemba 2006, pamoja na utangulizi wa Neville Alexanderr (Afrika Kusini/ACALAN) kupigia darubini maendeleo tokea mwaka wa 1997.

### Kanuni nne za Familia za Lugha za Kiafrika

Kulingana na mjuzi wa lugha anayetambuliwa kutoka Marekani, Bw. Joseph Greenberg, takriban lugha 2000 za Kiafrika zinaweza kupangwa katika makundi ya familia nne: **Niger-Congo, Afroasiatic, Nilo-Saharan na Khoisan**. Kukiwa na zaidi ya lugha 1,400 na takribani wazungumzaji milioni 360, familia ya lugha ya **Niger-Congo** ndiyo kubwa zaidi ulimwenguni kulingana na idadi ya lugha na ndiyo kubwa zaidi barani Afrika kulingana na idadi ya wazungumzaji. Lugha za **Afroasiatic** zinaunda familia kubwa ya pili barani Afrika (ikiwa na lugha 370), ikifuatiwa na **Nilo-Saharan** (karibu lugha 200), na familia ya **Khoisan** (lugha karibu 35). Nchi nyingi za Afrika zina aina mbali mbali za lugha, na mataifa yaliyo na lugha nyingi zaidi tofauti ni **Nigeria** na **Cameroon**, zikiwa na lugha 500 na 280 mtawalia. Lugha zinazozungumzwa sana, tukiacha lugha ya Kiarabu katika Kaskazini, ni Hausa, Yoruba, Igbo na Amharic; kila lugha kati ya lugha hizi inatumiwa na takribani wazungumzaji milioni 20 kama lugha ya kwanza. Kiswahili ni lugha ya familia ya Niger-Congo. Ina karibu wazungumzaji milioni 4 wa lugha hii kama lugha ya kwanza lakini inatumiwa na watu milioni 40 kama lugha ya pili, hasa Afrika Mashariki.

### Uwezeshaji katika juhudi za kuzilinda lugha za Kiafrika

Kitengo cha Turathi Zisizogusika, kwa usaidizi wa ACALAN, kilizindua mradi wa kuyapa nguvu mashirika ya kitaifa na kimaeneo kwa lengo la kuhifadhi lugha za Kiafrika. Mradi huu uliofadhiliwa na Serikali ya Norway, unaendeshwa kwa ushirikiano na idara za vyuo vikuu vya Afrika na asasi za utafiti zinazozingatia lugha za Kiafrika. Mkutano wa kwanza wa wataalam, uliopangwa kufanyika Machi 2006 huko Bamako, Mali uliwaleta pamoja wajuzi 50 wa lugha kutoka mataifa 26 ya Afrika na kutoa nafasi ya kuelezana na kufundishana kuhusu wanayokumbana nayo katika utafiti na kazi ya nje pamoja na kuimarisha ushirikiano. Mkutano wa pili, ambao utaangazia mafundisho bora ya kulinda lugha zilizo katika hatari ya kuangamia, umepangwa kufanyika huko Addis Ababa, Uhabeshi.

Kadhalika, juhudi za kulinda lugha tano za jamii ya watu wa Cameroon, Niger, Nigeria na Gabon ziliungwa mkono na UNESCO mnamo 2004/2005 (angalia mifano katika ukurasa wa 4 na 5).

# Taaluma Jumuishi



© Discovery Communications, Inc.

*Wabaka wapatao 5000 waishio Gabon wanajumuisha kundi la watu waishio msituni katika sehemu ya mpaka wa kaskazini mwa Cameroon. Tofauti na makundi ya watu waishio msituni ambao huzungumza lugha za kibantu, lugha ya Wabaka ni mojawapo ya nasaba za lugha ya Ubangi.*

## Sekta mbalimbali za miradi ya UNESCO za mipango zinajumuika kuendeleza uanuwai na upanuzi wa lugha

### Sekta jumuishi za UNESCO katika mipango ya lugha

Huku ikizingatiwa jukumu muhimu la lugha katika ujumla wa maisha na ukubalifu wa wote katika kuendeleza wingilugha na uanuwai wa lugha, UNESCO sasa iko katika kutayarisha mikakati ya sekta jumuishi huku Shirika hili likishirikisha mipango ya lugha iliyoko na ya baadaye. Mtazamo huu mpya jumuishi unahusu mipango na kazi kutoka katika sekta tano za Shirika hili:

**Kazi mahsusi katika Sekta ya Utamaduni**

- Kulinda lugha zinazohatarishwa na kuendeleza lugha kama njia ya turathi za tamaduni zisizogusika (Kitengo cha Turathi Zisizogusika);
- Kuendeleza fasihi na tafsiri, na kuwahimiza wachapishaji kuchapisha na kusambaza kazi katika lugha za kienyeji (Sehemu ya Shughuli za Kitamaduni na Hati miliki);
- Kuendeleza sera za kitamaduni (Kitengo cha Mfumo jumuishi na midahalo ya kitamaduni).

**Kazi mahsusi katika Sekta ya Elimu**

- Kuhimili elimu ya wingilugha na ufafanuzi wa vifaa vya kusomea/kufundisha pamoja na vitabu vya kiada kwa lugha za kienyeji (Kitengo cha Elimu kwa Amani na Haki za Binadamu);
- Kuendeleza jukumu la lugha za kienyeji katika mpango wa Kujua Kusoma na Kuandika ili Kujiwezesha – KIMAISHA (Sehemu ya Kujua Kusoma na Kuandika na Elimu isiyo Rasmi).

**Kazi mahsusi katika Sekta ya Mawasiliano na Habari**

- Kuhimili uanuwai wa lugha katika mtandao wa mawasiliano (wambiyo) (Kitengo cha Upatikanaji wa Habari na Uakibishaji);
- Kuendeleza lugha za kiasili katika vyombo vya habari na kujenga uwezo wa wazalishi wa habari hizo (Kitengo cha Maendeleo ya Mawasiliano).

**Kazi mahsusi katika Sekta ya Sayansi za Kiasili**

- Kuhimili lugha za kienyeji katika kupitisha ujuzi wa kiasili ( Maeneo ya pwani na janibu za visiwa vidogo – *LINKS*)

**Kazi mahsusi katika Sekta ya Sayansi za Kibinadamu na Kijamii**

- Kuchunguza na kuimarisha hali za kijamii za wingilugha (Kitengo cha Falsafa na Sayansi za Binadamu, Kitengo cha Haki za Binadamu na Maendeleo, Kitengo cha Mapambano dhidi ya Ubaguzi katika misingi ya Rangi).

Wasiliana na: Mauro Rosi, Kituo cha Sekta jumuishi za lugha, m.rosi@unesco.org

### Uanuwai wa Kiasili na Uanuwai wa Kiisimu – Uhusiano muhimu

Utafiti mwingi umefanywa kuhusu umuhimu kati ya uanuwai wa kiasili na kitamaduni. Taratibu za kiasili huweza kueleweka zaidi, kuhifadhiwa na kuendelezwa kwa kuzingatia tamaduni ambazo zimekuzwa kwa kujihusisha na taratibu hizo huku zikizitumia kwa njia endelevu, pamoja na kuziathiri na kuzibadilisha kwa mapana.

Tangu mwaka wa 2004, kitengo cha Turathi Zisizogusika kimehusishwa na shughuli za sekta mbalimbali kwa lengo la kulinda uanuwai wa kiasili na wa kitamaduni, hususan uanuwai wa kiisimu. Jamii nyingi za kiasili zimesheheni ujuzi mwingi wa mimea, wanyama, ikolojia na mifanyiko ya mifumo ya ikolojia. Ujuzi huu wa kiasili aghalabu huelezewa kupitia lugha zao. Katika mwaka wa 2004 na 2005, UNESCO ilijihusisha katika kuchunguza uhusiano kati ya uanuwai wa kiasili na uanuwai wa kitamaduni kupitia kwa miradi mingi ya nyanjani katika sehemu nyingi ulimwenguni. Zaidi ya haya, katika mwezi wa Aprili 2005 Sekta za Sayansi ya Kiasili na Utamaduni zilifanya mkutano wa pamoja wa wataalamu ili kutafuta njia za kudumisha upitishaji wa ujuzi wa kiasili kuhusu mazingira asili.

Tangu Septemba 2005, Kitengo cha Turathi Zisizogusika kimekuwa kikishirikiana na Afisi ya Utawala ya Maafikiano kuhusu Uanuwai wa Kiasili (UNEP) ili kukuza mwelekeo, hali na mienendo katika uanuwai wa kiisimu na idadi ya watu wanaoongea lugha za kiasili. Mwelekeo huu utasaidia kutathmini maendeleo katika kuhifadhi ujuzi wa kiasili kote ulimwenguni. Data kuhusu hali ya uanuwai wa kiisimu ulimwenguni ambayo itakusanywa na kuthibitishwa kulingana na masharti ya mradi huu, bila shaka itakuwa muhimu kwa shughuli za UNESCO zihusikanazo na Mkataba wa 2003 na uanuwai wa kitamaduni.

*Uwezo wa kutumia na kubadilisha mazingira, kujihusisha katika mazungumzo na kutangamana hutegemea zaidi ujuzi wa lugha.*
*Hivyo, kuwekwa pembeni au kutangamanishwa, kutengwa au kuwezeshwa, umaskini au maendeleo, yote hutegemea uchaguzi wa lugha.*

Koïchiro Matsuura, Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO

MCHAPISHAJI Idara ya Turathi za Tamaduni Zisizogusika (ITH)
Sekta ya Tamaduni, UNESCO
1 Rue Miollis
75732 Paris Cedex 15, Ufaransa
Barua pepe: ich@unesco.org
Kipepesi: +33 (0) 145685752

MHARIRI MKUU Rieks Smeets

JOPO LA UHARIRI Sabine Kube, Anahit Minasyan, Richard Lo Giudice, César Moreno-Triana, Fleur Perrier


MWANA-RUWAZA Jean-Luc Thierry

***Toleo la Messenger kuhusu Turathi Zisizogusika*** linapatikana katika umbo la chapa na elektroniki kwa Kiingereza, Kifaransa, na Kihispania.

Yote yaliyomo yanaweza kupakuliwa katika (www.unesco.org/culture/ich) na kupigwa chapa bila malipo ilimradi mwandishi atambuliwe.

Kwa maelezo zaidi kuhusu mpango wa lugha zinazohatarishwa:
www.unesco.org/culture/en/endangeredlanguages
Wasiliana na: Anahit Minasyan, a.minasyan@unesco.org
Sabine Kube, s.kube@unesco.org

turathi zisizogusika




© Conselho das Aldeias Wajãpi-Apina

## MACHAPISHO




Ramani ya UNESCO ya lugha za ulimwengu zilizo katika hatari ya kutoweka, na ambayo imeorodhesha kimaeneo takriban lugha 800 zinazohatarishwa, imezua mihemko miongoni mwa wasomi, wana habari na umma kwa jumla. Tangu kuchapishwa kwa ramani hii, UNESCO imepokea mwitiko kutoka katika jamii za lugha hizi na mamia ya makala kutoka kwa mashirika ya uchapishaji na kutoka katika sehemu mbalimbali za ulimwengu.

Kutokana na machapisho mawili ya makala (1996 na 2001) ya ramani, chapisho la wavuti la ramani hiyo iliyorekebishwa limeanzishwa, na limeanza na lugha za Kiafrika. Toleo la marekebisho ya ramani hiyo limepangiwa mwaka wa 2008.
Kwa habari kuhusu lugha zinazohatarishwa barani Afrika wasiliana na: www.unesco.org/culture/en/endangeredlanguages/atlas




Nchi kadha za Latini Amerika zina tajriba ndefu ya utekelezaji wa sera za kiisimu kuhusu lugha za kiasili. Ili kuangazia tajriba hizi na kupitisha desturi nzuri, Afisi ya UNESCO ya Havana ikisaidiwa na UNAMAZ, ambacho ni Chama cha Vyuo Vikuu vya Amazon, *Casa de las Americas* na afisi za UNESCO zilizoko Brasilia, Quito na Lima, ilitayarisha ripoti za sera za kiisimu huko Bolivia, Brazil, Columbia, Ecuador, Peru na Venezuela ambazo zilizingatia lugha zinazohatarishwa pamoja na masimulizi na vito vya kitamaduni. Ripoti hizi zilichapishwa kama kitabu na SIDII iliyoitwa *Lenguas y culturas en Amazonia. Diversidad en peligro?* (Lugha za Amazoni na Tamaduni. Uanuwai hatarini?), iliyozinduliwa rasmi katika Siku ya Ulimwengu ya Uanuwai wa kitamaduni kwa Mazungumzo na Maendeleo, Mei 21, 2006. Kazi hii inachanganua sera zilizoko za lugha na kusisitiza hatua ya haraka na ya pamoja ili kulinda lugha za kienyeji za Amazoni.
Wasiliana na: UNESCO Afisi ya Havana, Frederic Vacheron, f.vacheron@unesco.org

*(yaendelea kutoka uk. 1)*

Jamii za kisasa zinazidi kuwa na mtagusano; mipaka na mikingamo inapungua kila kukicha kwa sababu ya harakati za binadamu na maendeleo makubwa ya mtandao wa mawasiliano duniani. Hata hivyo, iwapo hakuna litakalofanywa, ulimwengu utakumbwa na athari mbaya ya kutoweka kwa uanuwai wa kiisimu, ambao utakuwa na athari mbaya kwa jamii husika. Wasorajua wa kupindukia wanasema ati ni kiasi cha lugha kama mia hivi ambazo ni kubwa, za kitaifa au zilizo rasmi ambazo zinaweza kufikiriwa kuwa salama.

Maendeleo ya hivi karibuni ndani na nje ya UNESCO yamepelekea kuwa na uelewa mzuri wa mambo muhimu kama vile:

- Mtagusano kati ya lugha, utamaduni na mazingira;
- Jukumu la lugha kama chombo cha turathi za tamaduni zisizogusika;
- Lugha kama chemchemi ya usanii na uanuwai;
- Jukumu muhimu la kuimarisha sera afiki za lugha ili kufikia Malengo ya Maendeleo ya Milenia, hususan, Elimu kwa Wote.

Kwa miaka kumi iliyopita, Kitengo cha Turathi Zisizogusika kimetekeleza shughuli mbalimbali zilizonuiwa kuchunguza na kuwasilisha suala tata la kuhatarishwa kwa lugha. Hili lilihusisha kuinua kiwango cha utambuzi wa watu kupitia uchapishaji na vyombo vya habari; kuhimiza miradi ya majaribio na kutambua desturi nzuri, hasa katika Afrika; kulinda lugha kama chombo cha turathi zisizogusika; na kuchunguza uhusiano wowote kati ya uanuwai wa kiasili na kiisimu. Njia hizi mbalimbali zimebainishwa kupitia kwa shughuli mbalimbali ulimwenguni na miradi ambayo imefafanuliwa katika chapisho la *Messenger la Turathi Zisizogusika*.

Utaratibu wa Umoja wa Mataifa haujaunda chombo mahsusi cha kulinda haki za lugha miongoni mwa makundi ya watu. Hata hivyo, kupitia kwa lengo kuu la UNESCO la kulinda usanii na uanuwai wa kitamaduni ulimwenguni, Shirika hili limechangia katika ukuzaji wa uanuwai wa kiisimu na wingilugha kupitia uteuzi wa vyombo shadidi katika mawanda ya utamaduni: Azimio la UNESCO kuhusu Uanuwai wa Kitamaduni la 2001, Maafikiano ya Kulinda Turathi za Tamaduni Zisizogusika ya 2003 na Maafikiano ya Kulinda na Kuendeleza Uanuwai wa Vielelezo vya Kitamaduni ya 2005. Katika moyo huo, sekta kadha za UNESCO zimeimarisha mipango inayohusiana na lugha, ambayo imevyaza mkakati mpya wa sekta jumuishi kuhusiana na lugha, ambao pia umefafanuliwa katika ukurasa wa 7. Kwa UNESCO, elimu ya uwili au wingilugha ni njia moja muhimu ya kuhifadhi uanuwai wa kiisimu na kutoa nafasi sawa kwa kila mtu bila kujali lugha yake ya kiasili.

Katika uhalisi wake, lugha zinazohatarishwa hulindwa kupitia kwa hatua zinazochukuliwa na mamlaka za kitaifa au kimkoa, kuandaa, kugharimia na kutekeleza sera zinazofaa. Aidha, ili kuweza kufanikiwa na kuwa na hatua endelevu, hatua hizi zitahitaji ushiriki wa jamii husika; hakuna lugha itakayoweza kulindwa au kukuzwa bila ya usaidizi kutoka kwa wazungumzaji wake.

Lingekuwa jambo bora iwapo nusu ya lugha zilizoko leo ambazo ni takriban 6,700 zingekuwa zinatumika kikamilifu kama vyombo vya mawasiliano na mihimili ya utambulisho kufikia mwaka wa 2200.

Shukrani ziliendee Shirika la UNESCO kwa jukumu lake la kuhifadhi uanuwai wa kiisimu. Utaratibu wa Umoja wa Mataifa sasa unaonekana uko tayari kuchangia katika lengo hili muhimu.